



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA



03.05.2023

### TAARIFA KWA UMMA

#### MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH 665,100,000 KWA AJILI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MSINGI KUPITIA MRADI WA BOOST

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba Ndg.Mussa Gama anapenda kuutarifu umma kuwa Halmashauri imepokea fedha za ujenzi wa Miundombinu ya shule za msingi ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kiasi cha **shilingi Milioni mia sita sitini na tano na laki moja (665,100,000)** ambazo zitatekeleza ujenzi wa miundombinu katika shule saba kwa mchanganuo ufuatao:-

1. Ujenzi wa shule ya msingi mpya Mambamba **Tsh.331,600,000**
2. Ujenzi wa madarasa mawili ya mfano ya awali shule ya Msingi Amani **Tsh.66,300,000**
3. Ujenzi wa madarasa mawili na matundu matatu ya vyoo shule ya msingi Chikongola **Tsh.53,100,000**
4. Ujenzi wa madarasa mawili na matundu matatu ya vyoo shule ya msingi Mjimpya **Tsh.53,100,000**
5. Ujenzi wa madarasa mawili na matundu matatu ya vyoo shule ya msingi Michenjele **Tsh.53,100,000**
6. Ujenzi wa madarasa mawili na matundu matatu ya vyoo shule ya msingi Majengo **Tsh.53,100,000**
7. Ujenzi wa madarasa mawili na matundu manne ya vyoo shule ya msingi Mihambwe **Tsh.54,800,000**

Fedha hizo za miradi zimeingia kwenye akaunti za shule saba ambazo zitatekeleza mradi huo na tayari maandalizi yameanza

Prisca Nsemwa

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba